**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Ardhi Iliyo Barikiwa Palestina**

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير

HIZB UT TAHRIR

**Ijumaa, 25 Jumada II 1446 H** | **27/12/2024 M** | **Na: BN/S 1446 / 19**

**<u>Taarifa kwa Vyombo vya Habari</u>**

# Ujasiri Wenu Kwa Mwenyezi Mungu, Enyi Madhalimu, Unatangaza Kukaribia Mwisho Wenu (Imetafsiriwa)

Wakati Mayahudi walipokuwa wakiizingira Hospitali ya Kamal Adwan mjini Gaza, kisha kuivamia, kisha kuichoma moto, na kuwapeleka wagonjwa, majeruhi, na wafanyikazi wa matibabu kwenye hatima isiyojulikana hadi wakati wa kuandika taarifa hii, badala ya mamlaka hiyo kulaani uhalifu wao, badala ya kuuchochea ulimwengu dhidi ya vitendo vyao viovu na vya kikatili, badala ya kuuhamasisha Umma wa Kiislamu kuwanusuru watu wa Gaza, badala ya kuona haya kwa heshima ya majeraha ya Gaza na Ukingo wa Magharibi, walikataa kufanya chochote isipokuwa kuwa Jenin, wakifanya matendo ya Mayahudi na kuwanyanyasa watu wa Palestina mithili Mayahudi wanavyowanyanyasa.

Baada ya saa sita usiku wa kuamkia Ijumaa, tarehe 27/12/2024, mwendo wa saa nane usiku, popo hao wa usiku walifyatua risasi kwenye nyumba ya Profesa Nimer Nassar kutoka Qalqilya, na risasi zikapenya kwenye mlango wa nyumba yake. Kisha, baada ya Swala ya Ijumaa, Mamlaka hiyo ya kihalifu ikamteka nyara, ili kwamba ujambazi wa usiku huo ukamilike kwa jinai ya mchana huo, na ili Mamlaka ya Palestina iweze kuthibitisha kwamba ndiyo inayowaachilia majambazi wake katili kwa watu wa Palestina.

Hapo awali ilifyatulia risasi nyumba kadhaa za watu wa Qalqilya, siku tatu zilizopita, na matukio haya ya kihalifu bado yanaendelea katika zaidi ya jimbo moja.

Wakati huo huo, mamlaka za kihalifu zilizosubutu kumkaidi Mwenyezi Mungu zilikuwa zikifanya uhalifu mwingine, kwani kikosi kikubwa kilivamia nyumba ya Mhandisi Muhammad Nidal Ayesh huko Artas - Bethlehem, lakini hawakumpata. Familia ya nyumba hiyo iliwaonya wavamizi hao juu ya hatma sawia na ya wafuasi wa Bashar, hivyo majibu ya wavamizi hao waovu yalikuwa ni kauli kubwa (Wamepotea katika nchi kinyume na mapenzi ya Mola wenu)! Wakaafikiana na kauli ya walinzi wao wa Kiyahudi waliosubutu kumuasi Aliye juu zaidi, Mwenyezi Mungu akawakasirikia na kuwalaani pakubwa.

Haya ni pamoja na matukio ya kipigo na udhalilishaji yanayofanywa na Mamlaka ya Palestina dhidi ya watu wa Palestina, ambayo vyombo vyake vya usalama vinayaandika na kuyachapisha ili kuwaambia watu kwamba nitawashambulia kama vile Mayahudi wanavyokushambulieni endapo mutatamka neno lolote, na mimi nitakuwa ni mkono wa juu wa Mayahudi katika kukupigeni. Lililo baya zaidi kuliko hilo ni kile ambacho zaidi ya mtu mmoja aliyekamatwa na Mamlaka ya Palestina ameripoti kuhusu baadhi ya wanachama wa PA kuendelea kumlaani Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Mtukufu awaulilie mbali!

Hivyo basi, Mamlaka ya Palestina na vyombo vyake vimeshuhudia mbele ya macho ya watu kwamba wao ndio waliolaaniwa, hawana tofauti na popo wa usiku na majambazi wanaowapiga risasi watu usiku, kutishia na hata kuharibu amani ya raia, na kutengeneza vifundo na chuki ambazo hazitaishia kwenye vyombo vya PA bali zitaiburuta nchi, Mwenyezi Mungu apishe mbali, kwenye moto ambao ni Mayahudi na makafiri pekee ndio wataufurahia na kutoa njia ya kufukuzwa kwa watu wa nchi kutoka humo.

Tunashangaa ziko wapi hizo taasisi za haki za binadamu zinazodai kunakili kesi za uvunjaji sheria, mashambulizi ya haki za watu, nyumba, na utu, na mateso magerezani?! Je, si kazi yao kusimama dhidi ya uhalifu huu na kuonyesha kwamba mamlaka, vyombo vyao, na majambazi wao wako nje ya “sheria”?

Je, ni lipi lengo la Mamlaka ya Palestina la kuwafanya watu wajae chuki dhidi ya vikosi vyake vya usalama? Je, lengo lake ni kupanua mzunguko wa mauaji? Takriban vikosi vyake vinne vya usalama vimeuawa, na watu wengi zaidi, na ni wazi kwamba viongozi wake wameazimia kuwazamisha watu wa Palestina ndani ya damu zao.

Ikiwa mamlaka hizo zinafikiri kwamba watanyamazisha watu na kuwatisha kwa uhalifu wao, wajidanganya. Jinai hizi huwachochea watu kuwa na chuki na hasira dhidi yao na mashirika yao, na kuwasukuma kutekeleza vitendo vya kulipiza kisasi dhidi yao. Kwa hiyo, tunatoa wito kwa wanachama wa vyombo vya usalama kufikiria kuhusu kile ambacho mamlaka inawasukuma kufanya dhidi ya familia na ndugu zao. Inatosha kwenu kuchukua funzo kutoka kwa wale walio karibu nanyi.

Ardhi Iliyobarikiwa ya Palestina ni nyumba ya Uislamu, na watabakia watu waaminifu humo wanaotangaza ukweli na hawaogopi lawama ya mtu yeyote kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wakijitokeza juu ya haki na wasidhuriwe na wale waliowaangusha.

Ama ujasiri wa wahalifu hao kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, unatangaza kukaribia kwa mwisho wao, na tunawapa habari njema za fedheha hapa duniani na Akhera. Hawakutafuta vita na watu wa Palestina, bali na Mola Mlezi wa watu wa Palestina, Mwenye Nguvu, Mlipaji kisasi. Hivyo, Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuwaangamiza na ndiye Mwenye kulipiza kisasi dhidi yao, na huenda hilo likawa karibu.

**[إِنَّ الَّذِينَ يُحَادُّونَ اللهَ وَرَسُولَهُ أُولَئِكَ فِي الْأَذَلِّينَ * كَتَبَ اللهُ لَأَغْلِبَنَّ أَنَا وَرُسُلِي إِنَّ اللهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ]**

**"Hakika wanao mpinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hao ndio miongoni mwa madhalili wa mwisho. Mwenyezi Mungu ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume wangu tutashinda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye kushinda."** [Al-Mujadila 58:20-21]

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir**
**katika Ardhi Iliyobarikiwa – Palestina**